Msimulizi, 1896[1]

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The perodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1896.

MSIMULIZI. 1896
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

KIUNGANI.

Dec. 12, tulifurahi sana kumwona Askofu wetu akija toka pande za Newala na Masasi, pamoja naye mwalimu Klementi Mkajanguya aliyekuwa akifundisha Masasi muda wa miaka miwili, na tena Isaya

[1] The text is issued under licence CC BY-NC

Mwalinjila na Benedict Njewa waliokwenda kutazama jamaa zao, na mwalimu wa Newala Petro Suleman, na mkewe mwalimu Leonard Pesa. Assubui yake ndio Dec: 13, alasiri tulipewa kucheza, (half-holday,) kwa furaha ya kusikia kama mwalimu Klementi huyu amefanywa Msomaji (Reader) huko Masasi Nov: 24, 1896.

Dec. 20, ilikuwa siku ya Chama chetu cha Paolo. Mt. saa a tatu u nussu ikawa sala ya "Litania ya kuwaombea mataifa," baadaye ikawa khotuba ya Askofu, na Padre Dale akifasiri kwa Kiunguja, maana Askofu, alitoa khotuba kwa maneno ya Kingreza. Siku kuu ya Thoma Mtume Dec. 21, tuliondoka hapa Kiunguni assubui mapema kwenda Mkunazini kwa maana Mr. Radford alitiwa Ukasisi siku hiyo katika Kanisa kubwa (Christ Church.) Vijili ya siku kuu ya Kuzaliwa kwake Bwana wetu, jioni yake ilikuwa sala kubwa kwa shangwi na uandamano, (procession) pamoja na khotuba. Askofu alikuwapo kwa sala hii, illa baada ya chakula akaenda Mkunazini illi siku kuu ya Christmas yenyewe awepo Kanisa kubwa, (Christ Church.)

MSIMULIZI. 955

Siku kuu yenyewe ya Christmas watoto waliamka assubui mapema kama saa a kumi wakaimba 'Carols' kwa kupokezana watoto walalao vyumba vya juu na walalao chini, ilipokoma saa edashara u nussu wakatulia. Bassi kengele za Usharika Mt. zikaanza, ilipotimia saa a thenashara u nussu, tukaingia Kanisani tukasali sala kuu ya Eukaristi Takatifu kwa shangwi mno sana, Padre wetu Mr. Dale akaaye mahali pa Archdeacon alitoa Eukaristi akisaidiwa na Mr. Bishop kusharikisha watu kikombe. Saa a nne ikawa tena sala ya assubui, na jioni yake ikawa sala ya shangwi kama siku mbele ya siku kuu yenyewe ya Christmas. Hivyo furaha ikaendelea.

Dec. 27, tulikwenda kushinda shamba mahali paitwapo Hatajwa, keshoye tukarudi zetu. Na mwenyi shamba tulilofikia jina lake Bwana Bakari, alitukaribisha sana kuliko tulivyothani kama Mwarabu ye yote angeweza kututendea; killa kitu tulipata burre katika shamba lake. Na Wazungu tuliofuatana nao ni Mr. Hitchborn na Mr. Faulkner, wakajaribu kumpa zawadi kwa wema aliyotutendea akakataa zawadi kabisa, akasema kwamba nimewakarimu tu. Tukamshukuru sana.

Jan. 1, 1896 wangine wetu tulikaribishwa Mbweni kwa harusi ya mwalimu Petro Suleman, na tulipokirudi magaribi kuja zetu hapa Kiungani pamoja na bwana harusi na bibi harusi, tukafurahi kusikia kama Rev. Samuel Sehoza, amekuja toka Magila

MSIMULIZI. 956

kwa matembezi, tulifurahi maana sisi wangine hatukumwona tangu siku nyingi kabla hajaenda Ulaya. Naye alikuwa akilala hapa Kiungani, na amekwenda zake Magila pamoja Bwana Askofu.

Jan. 17, mwalimu Kolumba Msigala na mwalimu Petro Suleman na mkewe wamesafiri kwenda Newala kushika kazi zao za kufundisha maana walikuja Unguja kwa kitambo tu. Na pamoja nao Wazungu wawili Rev. C. I. Radford, anakwenda Masasi, na Mr. Sim.

Padre Hood tangu ametoka, Newala alikuwa akikaa hapa, lakini akiwa tayari kurudi Newala akapata habari kama mamaye hawezi, naye yuko Misri, bassi sasa amekwenda huko Misri kumtazama na tunatumaini kumwona tena labda baada ya miezi miwili mitatu. Bibi yetu wa hapa Kiungani Miss Berkeley hawezi yuko katika Hospital huko Mkunazini.

Mwezi huu wa January ilikuwa "Exmination" katika School hii kwa darasa nne, I. II. III. IV. Bassi na walioshinda ni hawa: Darasa ya waalimu (ndio ya kwanza) wa kwanza Isaya Mwalinjila, wa pili Siluano Ngaweje, wa tatu Gabriel Ngalimasi. Darasa ya pili: wa kwanza Ohad Hamisi, wa pili James Mkumbano, wa tatu John Saidi. Darasa ya tatu: wa kwanza Stefano Kachinga, wa pili Denys, Sayite, wa tatu Cathbert Mlangwa, Darasa ya nne: wa kwanza Charles Mfuko, wa pili Geldert Senkoba, wa tatu Henry Semngindo.

MSIMULIZI. 957

Katika thawabu ya 'Examination' hii ilizidi sana kuliko siku zote, maana Mzungu mmoja Kasisi, Mr. Williams alitoa fetha kumpa Mr. Madan thawabu ya 'Examination' hii, naye alikuwa akitoka Cape, kusini ya Afrika; akienda Ulaya. Y. M.

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu, baada ya Salamu nakuarifu habari za hapa petu nazo chache tu.

Dec. 24, Siku ya Jumaa nne ilikuwa sala ya shangwi sana tulipita njiani tukiimba nyimbo za Uzaliwa. Hatta Dec. 25, ndiyo siku ya Uzaliwa wa Bwana wetu, shangwi ilizidi kabisa. Na watu wengi walipokea Eukaristi Takatifu. Dec. 26, Ndiyo siku kuu ya Stefano Mt. Kwa saa tatu tulikaribishwa na Miss Mills Kilimani kwenda kumwangalia Mhindi akifanya maajabu yake tukafurahi sana kiisha tukarudi kwetu.

Dec 27, Ndiyo siku ya Yohana Mt. Hatukwenda popote tulishinda hapa petu, hatta jioni ya siku ileile alibatizwa mtoto mmoja yule aliyetoka nyumba ya wagonjwa, jina lake Edith D. Jamile.

Dec. 28, Ndiyo sikukuu ya Wasiokosa, watoto wote tulikwenda kushinda Uwandani hatta mangaribi tukarejea nyumbani.

MSIMULIZI. 958

Jan. 1, Ndiyo siku ya Tohara ya Bwana wetu siku ileile aliolewa Thekla Siliwa na Petro Sulemani, tena siku ile Padre wetu alitoka kwenda pande za Mlima, na mahali pake akaja Padre Radford.

Jan. 5, Watoto kama kumi na mbili walikaribishwa mjini kwenda kuangalia Ubatizo wa mtoto wa Mwalimu Clara Kusi, hatta saa tatu ya usiku wakarudi nyumbani.

HABARI ZA KOROGWE.

Kwa Mtengenezaji wa msimulizi salamu, baada ya salamu na kuarifu kuwa hali yetu njema nalikuja kwako illi tuungane katika safari yetu ya kuwasumulia jamaa watutakao, lakini sijui kama nalitumbukia shimoni ao nimeingia katika kundi lingine sijui. Illa mwezi huu naja tena labda nitatafuta mchukuzi mwema zaidi ili nikufikie.

November 25 Mr. Chilvers alienda Magila kwa shughuli yake maana alitakiwa huko. Illa hakukawia kwani Nov. 28, alituwasilia tena alifuatana na Mr. Sanderson atokaye Unguja akija kwa matembezi tu.

Dec. 3, Mr. Chilvers na Mr. Sanderson wakaenda kwa Sigi wakarejea jioni December 6, alituwasilia Mzungu Mwingereza na karani wake Mdachi. Habari zake huyu bwana Mwingereza jinale ndio Mr. Martin. Amepelekwa kusudi na serkali ya Dachi kujua hakika

MSIMULIZI. 959

kama katika milki ya Wadachi imo thahabu ama sio. Sababu huko Ulaya Dachi kuna wangine wasemao kama kuna thahabu na wangine wasema sio bassi akachaguliwa huyu mzee, kwani kweli ni zee la Kingreza mvi chapa, bassi ni kushughulika kwenda vijitoni kuokota mawe ao kuchimbua mchanga, shughuli ni hiyo tu.

Dec. 17, Padre Chambers akaenda Mkuzi.

Dec. 24 ni siku iliyo mbele ya sikukuu ya Uzaliwa wa Bwana tukahamisha vitu katika kanisa jipya la mawe kwani limeisha juma ile ile mbele ya siku kuu jioni yake tukasali sala ya shangwi kwa dasturi ya siku kuu.

Assubui tukashika sikukuu kama ilivyo. Dec. 26, siku ya Stefano tukaenda kwa Sigi kushinda ikawa karamu barabara mchele, mbuzi mwema, sherbati; maandazi, biskuti, tende, killa aina. Jioni tukarudi nyumbani mwetu.

January 3, 1896. Bwana Martin akarejea alikokwenda illa alirudi na homa. Bwana huyu akija Kanisani mwetu killa jumaa pili alipokuwapo hapa, kwani alitua hema yake chini si juu hapa petu, illa nje ya mji wa Korogwe. Halafu yake homa ikamwacha. Hatta January. 6, huyu Bwana Martin na mwenzake wakaenda pande za Sigi, kwa shughuli yao. Watu wanalima tayari kwa kupanda mihindi ya mwaka. Illa nzige wamefunikiza inchi yote hii ya Zigua. A. J.

MWITI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Natumaini sana kama ulipata baina kidogo ya kuhama kwetu kule Chitangali, ukisikia hayo ni kweli. Tulipohama kule Mzee Barnaba Nakaam alikwenda zake Chiwata, mahali hapo papya alipohamia, lakini huyu Padre wetu hakwenda huko, maana alikuwa na shauri njiani mwake aliposikia barua ya Archdeacon ya kumwuliza kama anataka Shemasi. Na unajua ya kwamba huyu Padre alipokuwa kule Chitangali ilimlazimu kwa killa mwezi kuondoka Chitangali kwenda Miwa na Mwiti, bassi ilipotokea habari hii ya kuhama aliwaza hivi:

Mwiti imekuwa katikati ya mahali pale alipohamia Mzee Barnaba Nakaam na Miwa, bassi tulipohama kule Chitangali Padre akaja zake hapa pamoja na vitu vyake. Alipokuja hapa hakutenda lolote, hakuanza kujenga alikuwa akimngojea Askofu kumwarifu haya. Bassi alipokuja Askofu akamjuvya haya naye Askofu akakubali. Na waliposikia wamasihiya wa Chiwata wakakataa kuangaliwa tena na huyu Padre, wakamwambia Askofu heri akija huyo Rev. Hugh. S. Mtoka akae huku Chiwata asitazame kwa Padre Cecil, illa Newala ao Masasi.

MSIMULIZI. 961

Bassi naye Askofu amekubali hili shauri lao. Bassi sasa Chiwata imekuwa chini ya Masasi, na Miwa chini ya Mmwiti. Mkimwandikia Padre Cecil barua andikeni Mmwiti, lakini mkimwandikia Rev. Hugh andikeni Chiwata, huyu Rev. Hugh anakaa na mwalimu Daniel Usufu, na hapa Mmwiti tupo wawili mimi na Yohana Gilbert Mpalila.

Nathani ndugu zangu mtatusaidia kuhuzunika mkisikia kama shidda ileile ya mwaka jana na leo imetupata, shidda ya nzige.

Dec. 11, Mashamba yamefunikizwa na nzige na mwaka huu njaa imezidi kabisa kuliko mwaka jana, watu wamegeuka kuwa kama nyama kwa kula majani na kutembea mwituni kwa kutafuta matunda ya mwitu.

Kunako Dec, 14, safari yetu ya kutoka Lindi kuchukua mizigo ya Unguja ikafika hapa wakatuarifu kama Wadachi wamekwisha shuka Lindi na askari zao waenda kwa Machemba kupigana naye. Bassi kabla hawajaisha kusumulia, marra twamwona Mwenyi Barnaba Nakaam akitoka kwake Chiwata, kwani yeye alipata barua kwa Bwana mkubwa wa vita aliandika kabla hawajafika kwa Machemba kumwita wakutane kwa Machemba, bassi alikuwa na haraka sana ya kwenda huko, akakusanya watu wake na selaha zao akashika njia ya Chitangali kwenda kwa Machemba.

Na huyu Bwana mkubwa ni shemejiye Von Major Wissman, alitumwa naye kuja kumwangalia huyu Machemba hali yake, na jina lake Vantater. Bassi Machemba aliposikia kama Mdachi anakuja akatwaa mbuzi kumi na askari zake 200 wenyi bunduki, kwenda kumlaki kwa amani lakini hawa askari zake walikuwa na nia ya kupigana, bassi

MSIMULIZI. 962

Sultani Machemba akaondoka kwenda kukutana naye Vantater, bassi kabla hajaenda siku mbili tatu marra akutana naye, na hawa askari zake wakawa tayari kupigana nao, alipowaona waliotangulia, na walipowaona wote hapana mmoja aliyejipa kiume. Na Bwana mkubwa alipotokea akaona watu hawa na mbuzi hizi akauliza "Shenzi gani hii!" Akajibiwa ndiye Machemba huyu. Akamuliza wewe Machemba? Akasema Ndimi. Akasema tayari wewe kupigana na mimi! Akasema La, mimi nataka amani tu. Bass akajibu, Hakuna mimi nimekuja kukutia adabu kama wewe tayari kupigana nenda zako mjini kwako uwe tayari kwa mapigano, alipokwisha akaita 'Askairi', "Yaa" "Tumia mbuzi hizi." Tena akamwambia Machemba, jee umeleta watu wangapi hapa wenyi bunduki! Akajibu 200 Bwana, akasema waambie wakusanye bunduki zote walizonazo na pembe pia unipe. Kabla hajaisha kusema zimekwisha letwa, akampa ruhusa kurudi mjini. Akamwambia nitakaa hapa siku tatu kusudi ukatengeneze mji wako kwani nalisikia kama njia zote uliziba kwa sababu ya vita ya Makwangwara, bassi katengeneze, ukiwa u tayari kupigana ukazidi kuziba. Machemba akarudi zake kutengeneza mji, siyo kuzidi kuziba. Sikuya tatu Mdachi akaingia. Palikuwa na wazungu 16 na Manjolinjoli 411 na wapagazi wasio na hesabu kwetu siye.

Wakafanya mapatano kuacha jeuri na kuonea wenzake na kufanya vita, akakaa siku mbili. Bwana mkubwa mwenyewe na askari 141 na wazungu 7 na wapagazi wengi sana akazidi kwendelea kuja pande hizi kuangalia ginsi tunavyokaa. Na yule Mwenyi Barnaba Nakaam alikutana naye njiani kabla hajafika kwa Machemba kwani

MSIMULIZI. 963

ni kipande tangu hapa. Bassi siku ya Dec. 15, Saa sita wakatufikia hapa Mmwiti, watu waliuthika sana na hawa Manjolinjoli, na assubui yake Dec. 16, wakaondoka kwenda zao Lukulesi kwenyi ile Mission yao, na wamezunguka njia ya Rovuma hatta Mikindani.

Dec. 13, tumepata kengele kubwa toka Ulaya, ya hapa Mmwiti.

Dec. 13, Bartolomayo Mbinjika na Monika Mbinjika wamepata mtoto mume, akabatizwa Dec. 29, jina lake amerithi majina ya Padre aliyefia Nyassa, George Atlay. Na siku hii hii imeanzwa kutangazwa arusi ya Mwalimu Yohana G. Mpalila.

Dec. 30, mimi na huyu Yohana G. Mpalila pamoja na safari ya kwenda pwani kuchukua mizigo itokayo Unguja tukaondoka assubuhi na mapema, huyu Gilbert alikuwa akienda kununua vitu vya arusi yake na mimi kwa 'holidays' za Uzaliwa. Bassi tulipotoka hapa tukapumzika Chiwata tukapikia Pa Nambila tukaenda kulala kwa Makuwango, assubui tukaondoka tukaenda kupikia kwa Bwana Hasani tukaenda kulala Chilumbe, assubui tukaenda sana sana tukapikia kwa Mbaruku, na tulipotoka hapo ndio mpaka pwani soooo. Tulitoka hapa Juma a tatu tukafika pwani Juma a tano jioni, na njiani tukakutana nao Mwalimu Leonard. Mkwasomba na Edwin Ramathani wakirudi toka pwani. Tulipofika Lindi tukakuta askari wengi sana kama 500 wapo tayari wakiwangojea hawa wenzao waliopita pande hizi warudi wawe pamoja kwenda

MSIMULIZI. 964

zao kupigana na waume wenzao Makwangwara. Kwa sababu vita ile ya safari ya Che Nyambi iliyopigwa Masasi pembe zilizonyang'anywa zimekwenda kwa Dachi, bassi na hao Makwangwara wanawauthi sana watu wa Masasi. Wanasema kwa nini nyie ni watu wa Sonjela tena sasa mwageuka kushika mguu kwa Mdachi? Tupeni pembe mlizonyang'anya, kama sivyo wakati wa kula mihindi tu wageni wenu kuja kuwatwaeni mkakae kwa Sonjela. Bassi na Mdachi anakusanya askari zake kuwaendea washenzi hawa wasiovaa nguo kuwajuvya kama tangu wewe Sonjela mpaka wale wa Masasi ni watumwa wa Emperor. Bassi siku tuliyofika sisi pwani na hawa askari wa Vantater ndio siku waliyofika Lindi. Na siye tulishinda siku moja Jan. 1, ndio siku tuliyofika, tukashinda Jan. 2, na Jan. 3, tukaondoka kuja zetu tukalala siku tatu njiani. Jan. 7, tukawasili mjini.

Jan. 11, alitufikia hapa mfalme mmoja jina lake Maniamba alileta mhabari ya kuwa ameleta watu wake watatu, wa nini hawa? Padre Cecil awavushe hawa watu mpaka Unguja akaonane na Askofu wakamtake Mwalimu wa kukaa mjini pake. Lakini Padre alimwambia aandike barua tu kwa Askofu bassi ameandika barua kwa Askofu ya kumwomba Mwalimu, naye analeta watoto wake wawili kuja kusoma hapa Mwiti.

Natumaini sana ndugu zangu kama mtapenda mno kusikia (haswa nyie watu wa Mbweni) kama

MSIMULIZI. 965

kunako Jan. 12, ametufikia hapa ndugu yetu mmoja wa huko Mbweni alitoroka tangu zamani kufuata ulimwengu, lakini ulimwengu umempiga kofi na ameuona ulivyo. Alitoka Mbweni pamoja na mumewe mpaka Kilwa, bassi ameuzwa weee yapata hatta marra hamsini. Hatta Jan. 12, ametufikia hapa. Jina lake ni Maryamu Mrashi mke wa Timotheo Kombo, natumaini sana baadaye mtaonana naye kuko huko ajapo.

Jan. 16, tulikuwa na furaha kubwa sana sana tangu mto huu Mmwiti unapoanzia mpaka unapoingia katika Rovuma, tena tangu kuhamia hapa haijawa furaha ao shangwi kama iliyokuwa siku hii ya Jan. 16, Kwani ndio siku ya arusi ya Mwalimu Gilbert, Mpalila. Hatta watu walikuwa rathi kuacha kufukuza nzige katika mashamba kuja kushangilia arusi. Assubui mapema ikapigwa kengele ya sala ya assubui, na kunako saa tatu ikaanza kengele ya Ndoa Takatifu, alingojea hivi kwa kuwa watu wangine watokao mbali hawangewahi assubui mapema. Bassi ilipoanza kengele uangalie umati wa watu wajao, iliponyamaza tukaingia kanisani, lakini hakikuwaweka kwa kuwa kikanisa kidogo tu, kubwa bado kujengwa. Ikaanza taratibu ya Ndoa, na ilipokwisha Padre Cecil akakhutubu. Na tulipokwisha tukatoka, yakaanza kelele ya watu vigelegele na killa ghasia, bunduki zikaanza, zikapigwa weeee mpaka totolooo, kunako saa saba wakaponda mpunga kwa mbuzi na kuku, na saa za jioni ndio ikawa zamu ya Mzee Che Isaya Matonda

MSIMULIZI. 966

(kulya mtela) kucheza ngoma. Tena twashukuru sana Mwenyezi Muungu kwa kuwa bunduki tatu zikapasuka mikononi mwa watu lakini wasiumie, kwa kushindilia mno; moja ikampasukia Karlo Lisomba kwani alikuwapo naye hapa, na ya pili Benyamin Kalemwaga, na ya tatu Isaya.

Jan. 17, watoto wetu wawili Gideon Kawanga na Richard T. Kapili wamekwenda Newala kujiweka tayari kwa kwenda halafu Kiungani, kwa kuwa hapa tangu mwezi wa August hatta leo hivi hatujastarehe bado kwa kuanza kusoma, lakini Muungu akitujalia Jan. 24, tutaanza kawaida yetu kama kule Chitangali. Tafathalini ndugu zangu mlioko kote katika Upelekwa wetu tukumbukeni sisi tulio pande hizi za Rovuma, kwani watu wanakwisha kuta kwa njaa wangine wanauana kwenyi kwiba, imekuwa hatari kabisa mwaka huu tena shidda kubwa kwani hawa nzige ndipo wazidipo kuzaliana. Bassi ndugu zangu mtukumbuke katika sala zenu mbele ya Mola wetu. Leo tumepata habari kama Machemba amevushwa kwenda Dar-es-Salaam, hakika hatuna. P. H. M.

NEWALA.

Bwana Msimulizi twakusalimu. Tuna mengi kidogo tu kuarifu, kwani tumepitiwa kwa mwezi mmoja tusikuarifu. Bassi uwe radhi mno kwani mangine

MSIMULIZI. 967

tuyanenayo ni ya mwaka jana.

Dec. 9, nalianza kutazamia akili School ya chini mahameni. Tulianza mapema maana tulikuwa wawili tu, na katika chuo chetu hiki kikubwa zimo Darasa 8. Dec. 10, nalikwenenda chuo cha Mkanga nalilala kulekule asubuhi nikamaliza kazi hii ya kutazamia akili. Dec. 11, mnamo saa 8 nalizunguka kwenda kwa Akundonde chuo cha Mwalimu Filipo watoto wengi sana kule. Baada ya kuisha kazi ya kule nalirejea hapa. Dec. 13, tayari kwa Juma a tatu tuanze kazi ya hapa petu. Dec. 16, tulianza kazi hii niinenayo, ya Examination. Ilimalizika Dec. 19, Dec. 20, nalienda kwa Mripa, School ya Mwalimu Bartolomayo nikarudi 21. Dec. 24, ilikuwa Siri ya Ubatizo Mtakatifu kwa watoto 12 wa Nyumbani, majina yao ni haya. William Chiwalo, Andrea Mkalemaga, Robert Mtimbajila, Rafael Kunde, Nicholas Natika, James Mwambe, Guy Manyenje, Edward Likonja, Julius Ndaona, Isaya Monavai, Ethelbert Rausi, Francis Mkamuli.

Dec. 21, waliwasili Wadachi 7 na askari kathawakatha, jumla kombania 5, wengi wao wamerudi pwani kwani jumla tangu pwani walikuwa askari kombania tissa na wazungu tissa, wakimwendea Machemba, lakini isiwe vita. Bassi wangine wakamchukua Machemba mpaka Sudi karibu na Mikindani hatta sasa amefungwa huko kwa neno. Wangine husema atakwenenda Dar-es-Salaam kumwamkia

MSIMULIZI. 968

Von Wissmann na katika wale askari 900, 500 ndio waliendelea mpaka Masasi, na Chisanga, na hapa. Walitua chini mahame yetu ya zamani walikaa kama siku 3; Dec. 23, waliendelea pande za Rovuma wazunguke kumwangalia. Mgoni aitwaye Mkumba ndio hatta Mikindani. Kabla hawajaondoka hapa safari ingine ilitokea njia ya Mikindani, mzungu mmoja, baharia wa Kinyamwezi hawana idadi, pamoja na mfalme wa Kimakonde aitwa Chikambo. Takini yee alifukuzwa alipofika hapa, maana aliasi. Iliandikwa barua pia ya kusema bendera ipelekwe Lindi iliyopo mjini pake.

Dec. 21, Mwalimu G. Yohana Mpalila aliwasili hapa toka Mwiti. Dec. 22, Mwalimu Augustino aliwasili akitoka Miwa. Dec. 24, Mnamo saa sita za usiku, tuliamka tukaenda Kanisani ikatolewa Missa Takatifu mpaka saa 7. Tukaimba Carols kidogo tukalala. Assubuhi ya Uzaliwa tuliimba Carols tukizunguka mjini tukaingia Kanisani saa a kwanza mpaka saa 4 kasoro dakika kumi. Wamasihiya wengi hawakuwapo, wangine wagonjwa, wangine wasafiri hapa na hapa lakini jumla yetu tulioshariki siku ile tulipata 130.

Siku ile ya Uzaliwa watoto waliambiwa marks zao wakapokea haki zao. Walioshinda ni hawa: Class 1, Cuthbert Nyama, na Ambrosio Mtambarika. Class 2, Christofer L. Yakobo Mtopanyosa. Class 3, Bartolomayo M. Herbert M. Class 4, Alfred M. Joseph Teremu. Class 5, Klement Mitawa, William Chiwalo. Class 6, Rafael Kunde, Nicholas. Class 7, Julius Ndaona,

MSIMULIZI. 969

Isaya Monavai, Class 8, Riano na Monela. Walipoisha pokea zawadi zao walishindanishwa mbio, kuruka etc. Dec. 26, Mwalimu Filipo aliwaleta watoto wake wapokee zawadi zao walioshinda na wasioshinda pia. Mwalimu Bartolomayo M. pia na Mwalimu Marko L. pia, isipokuwa Mwalimu George S. kwani yee ni wa hapa. Dec. 28, Archdeacon Farler aliwasili hapa pamoja na Mwalimu James Chigulu kwani yee ni mgonjwa wa macho. Jioni yake watu walikusanyika nyumbani kuonyeshwa sanamu za taa Takatifu za Uzaliwa. Dec. 28, Watu wazima walikusanyika usiku kutazama mchezo wa Yoviniano Kaisari aliyejivuna. Uligawanyika kwa sehemu 7, sehemu 1. Kaisari aifikiri enzi yake aondoka aenda kuwinda. 2. Anania kaja kule msituni na nguo zachukuliwa na Kaisari mgeni. 3. Aenda kwa tajiri wa kwanza. 4. Aenda kwa tajiri wa pili 5 Aenda jionyesha kwa malkiya wake afukuzwa. 6. Aenda kwa Kasisi kutubu. 7. Arudishwa enzini mwake. Mwalimu Luke alikuwa malaika, mimi Yoviniano, Cuthbert malkiya, hatuna baina kama ulikuwa mzuri kwa sisi wachezaji labda kwa watazamaji.

Rev. Daudi ameanza kazi yake Dec. 2, 1895. Kawaida killa Juma atatu anakwenda zake na killa Juma amosi anakuja. Jan. 31, chuo, chake kimeanza tumiwa, ana watoto 32 wa daimara, wanafundishwa na Mwalimu Tomaso Juma. Na Padre amekuwa mtu wa kutembea sana kwa vijiji hivi vya Wamakonde vituzungukavyo, kwa hiyo twapata

MSIMULIZI. 970

wasikiaji wengi Juma a pili, na wapendao kujifunza zaidi pia wengi, Bassi hao huja Juma a nne.

Na nyumba yetu kubwa sasa karibu kuanguka, kwa hivyo tumehama tunalala chumba cha sermala na 'store room.' C. E. L.

MASASI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam: nakuarifu habari za huku kwetu inchi ya Masasi ya kwamba tumekuwa watu wa kutega masikio huku na huku. Bassi Sept. 30, Makwangwara walipita wakienda kwa Machemba. Bassi ikawa uthia mwingi na uwongo, marra wako mahali fullani, na wakati huu kazi zetu zikarudia nyuma kwani wakati mwingi ikawa hapana mafundisho kwa watu wazima ao kwa watoto. Kwani watoto wakapewa ruhusa kwenda kwao. Kwani hatukujua hakika ya hawa Makwangwara, wanakwenda wapi. Na vita hii wangine wakisema kama Mboani kaja analeta vita kwa ajili ya watu wa Masasi wamepiga safari ya watu wa Mataka bassi imewalazimu kuleta mateka ya vita kwa Sultani Sonjea, lakini kwa safari hii ikawa kuthani tu lakini walikuwa wakienda kwa Machemba, na Sept. 30, ndipo walipopita.

Na Oct. 2, akaja Bwana mkubwa wa Lindi jina lake Stannzler na karani wake mmoja. Na kusudi lake

MSIMULIZI. 671

kuja kutengeneza mambo ya vita kwani watu wakubwa waliandika barua kwa mkono wa Padre Carnon kusema sisi wakubwa wa Masasi tumekusanyika kwa mashauri, na tumepatana kama tu tayari katika vita hii akiwa mtu wa pwani tutamrudishia mali yake. Kwani vita si ya watu wa pwani illa Wayao. Bassi barua ilipofika pwani ndipo akatokea Bwana mkubwa wa Lindi kuja kutaka mali yote waliotwaa kwa watu wa safari, na mali yaliyotwaliwa katika vita hii ndio pembe, watumwa, na tumbako. Lakini barua ile iliandikwa pasipo kufikiri kwani wazee wetu hawajui kawaida za pwani. Bassi ikawaje? Kwani kufika kwa Satia tu Stannzler akaandika barua kwa Barnaba Nakaam kumtaka aje akutane naye kwa Tula, na Bwana mkubwa huyu alishuka nao askari 67. Na watu wa huku walipopata baina kama anakuja wakakimbia milimani wangine Mlasi ndiko kwenyi mashamba yao. Na watu wasiokimbia ni wa Mission. Na alimchukua mswahili karani wa kuandika barua za kiarabu jina lake Hasani wa Sumaili, na 'boy' wake Mhamedi, Mgazija wa Unguja. Saa kumi ilikuwa baraza kubwa umati wa watu usiyo na kifani. Na Majumbe 36 wa humu Masasi walikusanyika na mkubwa wa majumbe hawa ni jumbo Mkuti, na wapili Mkope, na Machinga, na katika mashauri haya waliokuwa tayari kukubali ni wa upande wa Mtandi na Chilonji, ndio wa pande za milima hii, wao walitoa pembe 6, na watumwa 3, na

MSIMULIZI. 972

mzigo wa tumbako, na mali haya Bwana mkubwa wa Lindi alimkabithi Mzee Barnaba Nakaam alete halafu Lindi, naye alishinda siku 3, na alipokuwa akienda akawaita majumbe 3 ndio hawa, Mkuti, Mkope, na Machinga akatoa zawadi kuwapa, na jumbe mkubwa ndiye Mkuti alimpa bendera akasimamisha uwanja wake. Na siku zilizoamriwa kuweka ndio Juma a pili na siku inapotokea safari. Akaisha akashika safari kwenda Newala assubui, na Barnaba N. akamchukua kwenda naye Newala na hatima Barnaba Nakaam akarudi, na mkononi barua ya majumbe na barua hii ikasomwa katika baraza ya Akumachinga akanipa mimi kuwasomea hawa majumbe, Na ndani ya barua ile mlikuwa na maneno mengi ya kusema kama hawakutenda kwa akili.

Kwa maana walikuwa na shauri moja kwa kupiga vita, lakini kwa mashauri ya kukusanya mali yote waliotwaa kwa watu wa safari hawakupatana. Kwani kusudi la kutaka wakusanye mali haya ndio warudishiwe wenyeji iwe amani killa inchi pasiwe ghasiya kama zamani za giza, kwani sasa karibu Afrika itakuwa nuru. Kwani twaona wale watu wa biashara walioingia zamani ndani ya Afrika wakati wa giza sasa wanarudi. Kwa nini wanarudi? Kwa maana nuru inaangaza ndani ya Afrika, nao waliokuwa wakizidisha giza ndio Waarabu. Lakini siku hizi wanarudi. Juzijuzi mnamo Dec. imepita safari ya Komakoma (Salimu bin Nasro). Lakini mwenyewe kafa Mtonya kwa ugonjwa

MSIMULIZI. 973

wa baridi yabis, na mali kakabithiwa mtumwa wake Kaluma wa Mandingo. Alipita na mali mengi sana kadri ya pembe 45. Na watoto wa Komakoma 7, waume 3 Na wanne wanaake, na mama yao. Na hawa wanapelekwa Masikati, na mali haya ndio masurufu ya kwenda kuhamisha mali yao. Na Manjawila kashuka yuko kwa Akumbemba na alipeleka frasila ya pembe kununua chakula afanye masurufu. Kwani huku kajaribu kununua chakula lakini kashindwa.

Nov. 4, ndio kurudi kwa Makwangwara katika vita yao nao wamekamata watu wengi sana. Kwa Machemba bin Mchakama hawakuwasilia kwani ilikuja fitina, kwa maana mtu aliyekwenda kutwaa vita ndiye Chiwalo akamwendea Machemba kusema kama Makwaligwara nimewaleta lakini wachache na twende tukawapige, nao watu wanasumulia kama hawa Makwangwara walitazama mazigambo yao wakaona kama huyu Chiwalo kawafanyia fitina kwa Machemba, bassi wakapiga vijiji 5. Tena wakawageukia Wamwela, kwani huyu Chiwalo ni Mwela. Bassi ilianza Mtua, pale ilipokuwa Mission, ikaendelea hatta Kwilondo hatta Luaha, ndio karibu na Lindi ndipo ilipokoma vita. Lakini watu wengi walioangamia. Naye Chiwalo alipoona walivyofanya hawa. Akalala akaamka akaona hapana shauri kwani alifikiri mji wa Abdalla Ngunde, na nussu ya miji ya Machemba na Wamwela. Bassi akajifisha binafsi yake kwa bunduki.

MSIMULIZI. 974

Dec. 8, Rev. Carnon juma a pili alikwenda Chiwata kuweka msingi wa nyumba ya Rev. Hugh. Kwani alipata barua ya Askofu kama Barnaba Nakaam kaahidi kama watu wake watajenga nyumba ya Padre wao burre pasipo gharama ya Mission. Bassi hatta nyumba hiyo bado wanaleta miti, naona kama shauri halikusimama, illa sasa Mission watanunua killa kitu nao watajenga burre. Dec. 17, Walikuja Wadachi 8 na askari 148 wakitoka kwa Machemba. Kwani wakati walipokuwa wakipigana na Makunganya Machemba akaandika barua kwa Bwana mkubwa wa Lindi kama nataka amani kwako wala mimi sasa si mtu. Na barua ilipofika Lindi Bwana mkubwa alikuwa Kilwa. Bassi wakaambiwa kama wangoje hatta arudipo huko Kilwa. Bassi aliporudi akasema kama Machemba uchague bandari yoyote utakayo, ukitaka Sudi, Mikindani, Kilwa, ao Lindi, bassi katika bandari hizi chagua mojapo. Bassi Bwana Machemba akawa mtu wa kutahayari niende bandari ipi? Tahamaki bwana amechelewa katika siku zilizochaguliwa, bassi akafunga safari kumwendea Machemba. Sikiliza bassi hila yake. Machemba akatwaa nguo zilizo bora zenyi majina ambazo nguo katika ulimwengu, na killa kijana asema nipishe mimi, baruti katika pembe killa kijana, ghala ikafunguliwa ya baruti kwani akasema Machemba wa Mchakama mimi huu ndio mwisho wangu naenda kwa miguu yangu nikaonane na kafiri huyu. Bassi akatwaa kaniki zilizo mbaya mbaya zilizotiwa mafuta akajitia, Bassi

MSIMULIZI. 975

katika hawa huwezi kupambanua Machemba kati ya vijana vyake illa kwa kuambiwa kama huyu ndiye Machemba, kwa ginsi alivyojigeuza. Naye ndio desturi yake Machemba huwezi kumfahamu ijapo akiwa mjini. Na mtu asiyepita mji wa Machemba atamkosea, kwani atamwona kama mtwana tu, kumbe ndiye Sultani. Bassi wakakutana njiani Mdachi anakuja na Machemba anakwenda, wakakutana njiani. Dachi wake askari 448 wazungu 12 na mkuu wa safari hii ni shemejiye Wissmann. Shauri Machemba? Akasema, tumekutana njiani, mzungu akasema twende mjini kwako, ndiko tutakakofanya mashauri ya kupatana. Njiani Mdachi akawauliza Waswahili yu wapi Machemba katika hawa? Akaambiwa ni huyu mwenyi nguo za kaniki.

Kufika tu mjini, marra Machemba yumo kifungoni na kifungo chake siyo cha kufungwa kwa mnyororo illa kwa amri, killa aendako na askari. Bassi tena kilichokuwapo mjini pake huwezi kunena kwa ginsi ya umati wa watu, mnajua kama askari wakikusanyika pamoja killa wakionacho hakina amri hula tu. Bassi akaambiwa lete bunduki zako zote, tahamaki marra zipo nyingi mbele yake, na mizigo ya bunduki imekwenda Lindi, bandera imekwisha simamishwa. Dachi akatoa makanda kumi ya mchele akampa. Akamruhusu akiwa na bithaa yake yoyote ruksa aende bandari yeyote atakayo kuuza, kiisha akaja zake huku barra ya Masasi. Askari 300, akawarudisha Lindi. Pamoja na wazungu 6, na wapagazi. Bassi

MSIMULIZI. 976

akaja hapa assubui na mapema wakaja na mdundo unalia, marra wakafika katika ua wetu, na marra boma limekwisha jengwa. Kiisha akaongea nao majumbe hawa maneno machache, Akasema mimi sina Shughuli juu ya mambo haya illa nimetumwa na shemeji yangu Wissmann kuangalia tu, kiisha akaenda Newala siku ya pili ndio Dec. 18,

Hapa alikuja Dec. 17, Akamwacha Mzee Barnaba Nakaam kutengeneza mambo hayo. Na watu wa Mkwela. Safari hii wametoa watu wengi sana kupeleka kwa Dachi ndio mateka waliyotwaa katika vita ile ya safari ya akina Mataka Aug. 23, 1895.

Dec. 23, Padre Hugh na watu wake walio Wamasihiya na wanafunzi wakaja kujiweka tayari kwa siku kuu ya Uzaliwa. Bassi jumaa nne saa a kumi ikawa shangwi kubwa baada ya sala Padre Hugh akahutubu.

Usiku saa a tissa unussu tukajaribu kujifurahisha kwa kuimba Carols mpaka assubui halafu yake panapo saa a kwanza ikawa kuanza sala ya Eukaristi Takatifu. Watu wengi sana walioshariki, wangine ukawa usharika wao wa kwanza, na tulitoka Kanisani mnamo saa nne. Baada ya sala ya pili ikawa mashindano ya mpira, wakubwa ndio Daniel na Alfred, na wa upande wa Daniel Usufu ukashinda, mkubwa wa kuamrisha machezo ni Mwalimu Petro Kilekwa. Na baada ya chakula cha saa sita, mashindano ya michezo kwa watoto, namna yoyote ya michezo na watu wazima

MSIMULIZI. 977
wa nje wakawamo katika michezo.

Na Alhamisi Dec. 26, ikawa kutawanyika tena killa mtu kwake na watoto wakapewa ruksa. Siku kuu hii mimi na Edwin tukaenda pwani. Penyi Nangoo nikapotea njia, kwani wenzangu naliwaacha mitini wakila matunda, nikafika mpaka ndani huko kwenyi mashamba ya akina Satia. Bassi nikakutana na watu nilipowauliza njia yangu wananijibu sivyo tu, eti wewe mtoro? Kujaribu kusema kama nilivyoweza isiwezekane, tamaa yao wanile tu, fetha mkononi nikatoa kunionyesha njia mpaka kwa Edwin isiwezekane. Nussura ya kuingia mnamo kongwa, Ah wasema kaa mpaka jioni ndio tutakupeleka, marra wakatokea akina Edwin wakinitafuta kwa bidii. Hii ndio tamaa ya washenzi.

Juma a tatu tukawasili Lindi, Juma a tano tukashuka tayari kurudi. Tulipofika kwa Satia tukasikia kama mtu amekufa alikuwa akiiba kwa Wamakonde akapigwa bunduki. Siku hizi njaa nzito sana wengi wanakufa kwa njaa na walio na chakula wanapigiwa bunduki. Nzige wanazidi sana bassi tutupieni msaada kwa sala angao nzige waondoke.
L. M.

MSIMULIZI. 978

SAFARI TOKA UNGUJA HATTA NYASA.

Salamu sana kwa Mtengenezaji, baada ya salamu, naona ndugu zetu, mtapenda sana kusikia habari za safari yetu.

Bassi panapo Sept. 24th, 1895, tulifunga safari. Ndugu zetu walitupeleka hatta melini pamoja na mwalimu wetu Bwana Hitchborn. Assubui ndio tukang'oa nanga, tukaenda siku tatu baharini, siku ya Sept. 27, tukawasili Msumbiji tukalala siku moja, assubui yake tukaingia katika Peters meli ndogo itumikayo pande hizi za Chinde.

Bassi meli kubwa ndio Kaiser, ilitangulia kung'oa nanga, ilienda pande za Natal, bassi panapo saa tatu, tukang'oa nanga tukafika Quilimane Sept. 30, alasiri. Bassi Bwana Faulkner, akasema heri wangine wenu washuke pwani kununua masurufu, bassi tukaenda pamoja na Wazungu wetu wote watatu tuliofuatana nao kuja kutusayidia ndio Bwana Faulkner, Misses A. Rees, na Ellershaw, pamoja na mzungu mmoja wa Serkali, naye ni mkuu wa askari, alikuwa akikaa Hindi, anajua sana Kihindi.

Sasa amekuja huku Nyasa kwa kazi yake ya askari, kweli ni askari, kwani mtu wa kutiisha sana. Bassi huyu jemadari jina lake, Captain DeWinton, bassi tukashuka, tukatumaini kama tutapata mahitaji yetu kumbe wapi, tulipokwenda sokoni hatukukuta kitu illa visamaki na nazi, bassi tukanunua samaki tu, tusipate kitu kingine bassi kazi ilikuwa kutembea

MSIMULIZI. 979

madukani tu bass. Bassi tukajaribu kuvunja rupia, ache tusumbuke, killa tuendapo inakataliwa kwa sababu rupia zitumikazo huku zimepigwa chapa, bassi tukajaribu killa duka mwisho kwa bahati tukavunja. Quilimane ni mji mzuri kwa upande wake lakini haupiti Msumbiji, bassi watu wa hapa hawajui kuvaa, hawavai kama tunavyovaa sisi hupenda sana kuvaa winda, nao ni Wamakua na Wachikunda, wote karibu husema Kimakua, shidda sana kumkuta ajuae Kiswahili hatta Wahindi pia husema Kimakua kitupu.

Bassi panapo saa a kumi na moja tukarejea tena melini.

Panapo Oct. 2, tukang'oa nanga kwenda Chinde, tukalala mlangoni pa mto Kwakwa, kwani ndio bandari ya Quilimane, kwani tulitoka alasiri saa kumi, assubui tukang'oa nanga, ndio Oct. 8, tukafika Chinde. Lakini nimesahau neno moja katika Peters tukakarimiwa na Nakhodha wake, alitupa gunia moja la mchele, tulimshukuru sana kwani tulishinda siku mbili pasipo chakula na huyu Nakhodha alijuana na Bwana Faulkner tangu Ulaya.

Bassi turejee Chinde, tunajua wote kama ndio inchi ya Wareno, bassi na Waingreza wana sehemu ndogo sana mahali hapa ni pazuri sana na bandari yake ajabu, ndio ginsi mji huu, unavyostawi upesi. Safari ya kwanza ndio 1892, twaliona nyumba hapana kabisa wala nyumba za watu wa asili hazikuwapo,

MSIMULIZI. 980

lakini sasa zipo, tena Wazungu wanazidi sana sana kuzijenga nyumba za mabati, tena hii ndio bandari kubwa ya (Central Africa).

Jambo moja liuthilo watu hapa ndio ugonjwa wa matekenya, hawa matekenya wameenea sana pande hizi za Nyasa, wadudu hawa wamekuwa kama viroboto kwa aina yao, hupenda sana kuingia nyayoni na vidoleni kuliko mahali pangine, kwanza wanapanda usipojua bassi ukiwaondoa hapana kitu, lakini ajapo ukiwaondoa wangine huingia upesi sana wala huwezi kumwona illa baada ya siku tatu, utaona anawasha kama umechomwa na shindano vile, na ukitumbua, utamwona amekuwa mkubwa, wala hungemtambua kama ndiye kwani ni kitu kidogo sana, bassi utaona kama njugu mawe, amekuwa mweupe kama karatasi, na ndani yake ndio mayayi, na ngozi yake ngumu kwa kadri, bassi umuapo, pasipo kumtumbua, ndio itakuwa heri, kuliko kumtumbua; hapana wadudu wakali kuliko hawa kwani huingia ndani kabisa na umtoapo damu hutoka ovyo. Bassi tulipofika hapa Chinde tulipatikana sana na ugonjwa huu, bassi aacha tuuthike baadaye wala hatukuweza kwenda vema, wangine tumefika nao. Huku pande za Nyasa, na Chinde, na Zomba, watu wengi sana wanakwenda pecha, hawawezi kwenda vema.

Tulifurahi kumwona ndugu yetu, ndio Philip na Reginald kwani wanafanya kazi hapa Chinde. Lakini

MSIMULIZI. 981

tulipofika tuliambiwa habari ya kufa Bwana Askofu pamoja na Bwana Williams, na kuuawa Bwana A. Atlay, tulistuka sana kusikia habari hizi pamoja na huzuni. Kwani wote tulifurahi sana tuliposikia habari za kupatikana Maaskofu: tena tulipomwona Askofu Maples akija pande hizi za Nyasa tulifurahiwa kama anakwenda kufanya kazi yake kumbe sivyo. Tena karibu wazungu wetu wote walikata tamaa walitaka kurudi kwao Ulaya, illa Bwana Faulkner aliwatuliza, akisema "Haithuru twendeni kuko huko Nyasa."

Habari za kuzama mashua na zingine mtasikia katika habari za Kotakota. Bassi panapo Oct. 8, tulitoka Chinde tuliingia katika Stevenson meli ya mtoni.

Panapo Oct. 11, usiku mzungu mmoja alianguka majini, marra mashua zikafunguliwa wakamtafuta, wakamwona, watu wa melini wakafurahi, ndiye yule yule mkubwa wa askari alitumbukia marra mbili. Panapo Oct. 12, tulifika Misonjwe ao Pinda Kijiji cha African Lakes Company. Bassi mahali hapa ni pabaya sana kwani mto umegawanyika, na maji yake yanakwenda kasi, naona mto Shire. Bassi Captain akasema kama mashua zote zifunguliwe. Bassi zikafunguliwa, meli ikaingia ndani, nasi tukajaribu kupitisha mashua tukapitisha kwa shidda sana, kumbe mbele yake maji yalikuwa haba sana bassi ilikuwa kazi kubwa sana kukokota mashua kwani zilikuwa na shehena

MSIMULIZI. 982

tukajaribu sana kwa nguvu bassi tukafika pwani, kazi yetu ilikuwa kutafuta masurufu kwanza, na masurufu yenyewe ndio viazi kwani watu wakaao pande hizi hupenda sana kulima viazi.

Bassi tukanunua, tukala tukaisha. Ilikuwa kazi ya mabaharia kuondoa mizigo, na kupeleka pwani illa kupunguza shehena katika meli kwani hakuweza kupita, kwani maji yamepunguka sana, bassi ilikuwa ya wakati mwingi.

Panapo alasiri siku ya pili yake shehena ikapunguka mwenyi meli, bassi wakaita watu wengi kukokota meli kama nilivyosema kama maji ni haba kabisa, bassi huku watu wameshika kamba na mashini inatenda kazi, kwa bahati ikapita ikafika penyi 'Station' haswa, na mizigo ilitolewa pamoja na yetu, iliwekwa mbali kabisa kama mwendo wa nussu saa, zile mashua zilikuwa zikipakia, zikipeleka kwenyi meli kwani zilikuwa mashua mbili kama nilivyosema, na sisi wote tulikuwa kule kule kwenyi mizigo, zikapakia marra mbili na marra ya tatu, ndio kumaliza mizigo yote iliyobaki. Bassi mzungu huyu wa hapa Pinda alikuwa mkaidi, akapakia mizigo yote. Na nussu ikabaki bassi akatuambia chukueni wenyewe nasi tukakataa, bassi palikuwa na mtumbwi, akasema pakieni humo mtumbwini, tukapakia vyakula vyote na mikeka, bassi tukatoka, na mle ndani ya mtumbwi aliingia William Mpota na mwenyewe, bassi wao walitangulia, na mashua zote mbili zikafuata

MSIMULIZI. 983

nyuma. Bassi tukaenda marra tukaona kuku na mtumbwi na mikeka vinaelea, na William akicheka pwani, na mwenyi mtumbwi akipiga kelele. Bassi kwa kuwa mtoni naswi tulikuwa tukipanda, vile vyote vikachukuliwa na maji, ndio hasara iliyotupata, tangu siku hiyo, hatukujua kulalia mikeka, illa chini. Ulipozama mtumbwi ndio Oct. 14,

Siku ile ile tukatoka, na panapo Oct. 16, tukafika mlima wa Mbona. Huyu Mbona wenyewe husumulia kama alikuwa mtoto wa mfalme wao (watu wenyewe ni Wachikunda, kwa asili Wanyasa.) Bassi akatoka mjini akaenda kukaa katika milima hii, tena husema kama ni mtu mweupe kama mzungu, tena hapendi kuonekana na watu wala wazungu: husema kama mzungu mmoja tu ndiye aliyepata kumwona, ndio maana huitwa milima ya Mbona. Panapo Oct. 16, tukafika Port Herald. Tukafurahi sana kumwona ndugu yetu Mattayo Lamilako, alitukaribisha, tena tulikuwa tukilala kwake, watu wa hapo humheshimu mno, humwita Bwana, kwani ndiye mkubwa chini ya mfalme ndiye akataye maneno, naye yu katika kazi ya Serkali, ndiye aliyewekwa kuwa mlinzi wa mji, na kuangalia killa jawabu.